# ARUSHA TECHNICAL COLLEGE

*Skills Make the Difference*

## UFUNDI BULLETIN

TOLEO LA NNE







**BODI YA ATC YAPONGEZA HATUA UJENZI WA MRADI WA KUFUFUA UMEME-KAMPASI YA KIKULETWA**



*Mwenyekiti wa Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi Arusha (Katikati) akiwa kwenye picha ya Pamoja na Wajumbe wa Bodi wa Chuo hicho walipotembelea eneo la ujenzi wa mradi wa kufua umeme kampasi ya Kikuletwa*

*Na Mwandishi wetu*

Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) kimepongezwa kufuatia usimamizi mzuri wa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme unaojengwa katika Kampasi ya Kikuletwa iliyopo wilaya ya Hai mkoa wa Kilimanjaro utakaotumika kuzalisha umeme na kutoa mafunzo kwa vitendo.

Akizungumza baada ya kutembelea mradi huo Mwenyekiti wa Bodi ya Utawala ya Chuo cha Ufundi Arusha Dkt. Noel Mbonde amepongeza uongozi wa Chuo kwa usimamizi mzuri katika hatua za ujenzi wa mtambo huo.

"Nawapongeza Bodi ya Chuo ambao wamekua wakifanya kazi bega kwa bega na uongozi wa Chuo kuhakikisha kwamba mradi huu unaendelea kama ulivyopangwa, inabidi tuendelee na huu utaratibu wa kutembelea miradi, sio huu tu bali miradi yote ya Chuo cha Ufundi Arusha" alisema Dkt. Mbonde.

Vilevile Dkt. Mbonde amemshukuru rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha za ujenzi wa kituo hicho.

"Nichukue fursa hii kumshukuru rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki, na pia shukrani nyingi ziwaendee viongozi wetu wa Wizara kwa kusimamia kwa makini sana maendeleo ya ujenzi wa kituo hiki" alieleza Dkt. Mbonde.

Aidha Dkt. Mbode alifafanua kwamba lengo la mradi huo ni kusaidia kuzalisha umeme Kwenda kwenye gridi ya taifa na pia utatumika kama kituo cha mafunzo ya uzalishalishaji wa umeme kwa wanafunzi watakaosoma fani za mafunzo ya umeme.

Mtambo huo wa kufua umeme unajengwa kupitia mradi wa Afrika Mashariki wa kujenga



ujuzi kwa mlingano na uingiliano wa Kikanda (EASTRIP) kupitia fedha za Benki ya Dunia ambapo mpaka sasa umefikia 77% kwa awamu ya kwanza na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba.







# ATC YAENDESHA MAFUNZO KWA VITENDO KWA JESHI LA WANANCHI KWENYE FANI ZA UJENZI

*Na Mwandishi Wetu*



Mafunzo kwa vitendo ndio kipaumbele kikubwa kinachozingatiwa kwenye ngazi zote za mafunzo yanayotolewa Chuo cha Ufundi Arusha. Katika kuthibitisha hilo Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) kinaendesha mafunzo kwa vitendo kwa jeshi la wananchi Tanzania katika fani za ujenzi, kupaka rangi na useremala.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo hayo, mhandisi Elineema Msuya ambaye ni msimamizi wa mafunzo amesema kwamba mafunzo hayo yameshaanza na yatafanyika kwa wiki nane.

"Mafunzo yameanza na yamegawanyika katika Makundi matatu, kuna vijana wanaojishughulisha na upakaji rangi ambao wapo vijana 15, pia tunao vijana wanaojishughulisha na useremala wapo 14 na tunao vijana wanaojishughulisha na ujenzi ambao wapo 21, mafunzo yanaenda vizuri na yatafanyika kwa wiki nane" alisema Mhandisi Msuya.

Aidha Mhandisi Msuya aliongeza kuwa kutokana na uwepo wa vifaa vya kisasa na miundombinu bora ya kujifunzia iliwafanya jeshi la wananchi Tanzania kuchagua Chuo cha Ufundi Arusha kuja kufanya mafunzo ya muda mfupi kwenye Chuo hicho.

"Jeshi la Wananchi Tanzania linahitaji vitu bora na katika kutafuta vitu bora waliona ya kwamba elimu inayotolewa Chuo cha Ufundi Arusha kwa upande wa ujuzi ni nzuri na inatoa ubora unaokubalika ndio maana wakaona wakishirikiana na Chuo hiki watapata vijana wenye ujuzi wa kutosha wa kuweza kufanya kile ambacho taifa linawategemea kufanya" alieleza Mhandisi Msuya.

Franc Mganga ni mwanafunzi kutoka Jeshi la Wananchi aneyeshiriki mafunzi hayo ambapo anaeleza kwamba



kwa kiasi kikubwa mafunzo yake anayapata kwa vitendo na sehemu ndogo iliyobaki ni nadharia ambayo wanafundishwa darasani.

“Nafurahia sana haya mafunzo kwa sababu kwangu imeniongezea morali ya kujua mambo mengi zaidi, kipindi cha nyuma tuliwahi kujifunza lakini hatukupata mafunzo mazuri kama hapa ambapo tunayapata kwa nadharia na vitendo” alieleza Franc

Naye Caroline Maluchila, mshiriki wa kike kwenye mafunzo hayo ametoa wito kwa wasichana na wanawake walioko kwenye fani za ufundi wasijisikie unyonge na badala yake wachangamkie fursa za mafunzo zinazotolewa na Chuo cha Ufundi Arusha.

Chuo cha Ufundi Arusha na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kupitia Shule ya mafunzo ya Uhandisi (SOFE) waliingia makubaliano ya kushirikiana kwenye eneo la utoaji wa mafunzo ambayo hufanyika kila mwaka. Lengo la mafunzo ni kuongeza ufanisi wa watumishi wao kwenye fani mbalimbali za uhandisi







## SHULE YA SEKONDARI PATANDI MAALUMU YAFANYA ZIARA YA KIMASOMO ATC




*Na Mwandishi Wetu*

Katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo ziara za kimasomo huwa ni chachu ya kuchagiza uelewa wa wanafunzi kutoka kwenye nadharia walizojifunza darasani. Shule ya Sekondari Patandi Maalumu imetembelea Chuo cha Ufundi Arusha ili kuwaonesha wanafunzi wake baadhi ya mafunzo kwa vitendo yanayotolewa chuoni hapo na fursa za kujiunga na chuo hicho.

Akizungungumza wakati wa ziara hiyo Mwalimu Mkuu wa shule ya Sekondari Patandi Maalumu Bi. Janeth Mollel amesema lengo la ziara hiyo ni kupata fursa ya kuona mafunzo yanayotolewa na kujua vigezo vya kujiunga na Chuo.

"Lengo za ziara ya kutembelea Chuo hiki cha Ufundi Arusha ni kuwapa wanafunzi fursa ya kujifunza program mbalimbali zinazotolewa hapa chuoni, kwa mfano tuna Watoto viziwi, tuna Watoto wasioona, tuna Watoto wenye ulemavu wa ngozi, tuna Watoto wenye usonji, lakini pia tuna Watoto wenye ulemavu wa akili, tumewaleta ili wajue baada ya kumaliza kidato cha nne wasihangaike, wajue chuo kina programu nyingi wanazoweza kusoma" alisema Bi. Janeth.

Aidha Bi. Janeth aliongeza kuwa wakati mwingine Wanafunzi hao wakimaliza



shule wanakosa mwelekeo wakasome nini lakini ziara hii imewawezesha kutambua fani mbalimbali wanazoweza kujifunza ikiwemo uhandisi magari, uhandisi umeme, uhandisi ujenzi, uhandisi mitambo na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Naye mwanafunzi wa Shule hiyo Maalumu Jilabanja Mange amesema amejifunza mambo mengi kwenye ziara hiyo ambayo yatamsaidia kwenye maisha yake.

“Nimejifunza mambo mengi kwenye ziara hii, Chuo hiki ni miongoni mwa vyuo bora kabisa Tanzania, nimetembelea karakana zote nimeona miundombinu iliyopo ambayo inaruhusu pia hata wanafunzi wenye ulemavu kushiriki mafunzo bila shida yoyote” alisema Jilabanja.

Shule ya Sekondari Patandi Maalumu ni shule ya serikali na jumuishi ambayo inachukua Watoto wenye mahitaji maalum kama vile viziwi, walemavu wa Ngozi, usonji na ulemavu wa akili.

> “Nimejifunza mambo mengi kwenye ziara hii, Chuo hiki ni miongoni mwa vyuo bora kabisa Tanzania





